JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA

# SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA

ISO 9001:2015 Certified

*Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali*

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MADAI YA UWEPO WA DAWA ZA MENO ZENYE VICHOCHEO VYA KIBIOLOJIA (*HORMONES*)

**Dar es Salaam, 01 Aprili, 2023**

Hivi karibuni, kumekuwepo na taarifa inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii inayoelezea uwepo wa dawa za meno zinazotolewa kama msaada katika baadhi ya shule hapa nchini zinazosadikika kuwa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) tumepima na kuthibitisha zina viambata ambavyo ni vichocheo vya kibiolojia (*hormones*) vinavyoathiri watumiaji hasa watoto wa kiume.

TBS inakanusha maelezo ya kwenye ujumbe wa maneno unaosambaa kwenye mitandao ya kijamii kuwa ilipima bidhaa hizo za dawa za meno na kutoa taarifa kuwa zina vichocheo hivyo vya kibiolojia.

Aidha, TBS baada ya kupata taarifa hiyo imefanya ukaguzi na uchunguzi wa awali katika bidhaa husika na kugundua hakuna uwepo wa vichocheo hivyo vya kibiolojia.

Hata hivyo TBS inaendelea kufanya ufuatiliaji wa suala hili kwa kushirikiana na maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

TBS inawashukuru wananchi wote ambao wanaendelea kutoa ushirikiano kwani suala la udhibiti wa usalama na ubora wa bidhaa ni mtambuka (*shared responsibility*).

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia kituo cha huduma kwa wateja kwa namba hiyo **0800110827.**

Imetolewa na:

Gladness H. Kaseka

**MENEJA UHUSIANO NA MASOKO**


**TBS MAKAO MAKUU**
Shirika la Viwango Tanzania
Barabara ya Sam Nujoma / Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam
S. L. P. 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu Na: +255 22 245 0298/ +255 22 245 0206
Nukushi: +255 22 2450959
Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: http://www.tbs.go.tz
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya wateja: malalamiko@tbs.go.tz
Twitter: TBS_Tanzania
Instagram: tbs_Viwango

**TBS KANDA YA KATI**
Jengo la Kambarage
S. L. P. 2956
DODOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 26 2520310

**TBS KANDA YA ZIWA**
Jengo la NSSF, Ghorofa ya 3
S. L. P. 1814
MWANZA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2505044

**TBS KANDA YA KASKAZINI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 2399
ARUSHA, TANZANIA
Simu Na: +255 27 2520143

**TBS KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7
S. L. P. 1674
MBEYA, TANZANIA
Simu Na: +255 25 2502848

**TBS KANDA YA KUSINI**
Jengo la MTUWASA
S. L. P. 1396
MTWARA, TANZANIA
Simu Na: +255 23 2334477

**TBS KANDA YA MAGHARIBI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 1276
KIGOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2804023


Barua zote ziandikwe kwa **MKURUGENZI MKUU**